

HOTUBA YA WAZIRI MKUU KWENYE UZINDUZI WA TOVUTI ZA MIKOA MKOANI KILIMANJARO TAREHE 19 FEBRUARI 2009

Dhana ya upatikanaji habari na taarifa ni pana. Haki ya kutafuta, kupokea na kusambaza habari ni haki ya msingi kwa binadamu wote. Katika swala zima la uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi na upatikanaji wa taarifa dhana hii iko kikatiba (Ibara ya 18(2)).

Katika kutekeleza hili, Serikali iemanzisha vitengo vya Habari , Elimu na Mawasiliano katika Wizara zote ili sera , mikakati na utekelezaji wa shughuli za Serikali uweze kuwafikia wananchi. Swala la msingi ni kuongeza mawasiliano ya shughuli za serikali kwa wananchi.

Maendeleo katika teknolojia, hasa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) ni fursa ya kutekeleza dhana nzima ya mawasiliano ya uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi wake. Ni fursa nzuri ya matumizi ya TEKNOHAMA katika kutekeleza majukumu ya serikali kama vile kupanga, kuandaa bajeti , kusimamia utekelezaji na kutoa taarifa (serikali mtandao).

Ilani ya uchaguzi ya CCM (2005) inaelekeza pamoja na mambo mengine maswala tafuatayo:

- o Kutoa Tanzania kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea.
- o Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha na kuongeza uwazi katika bajeti ya Serikali kwa kuhakikisha sheria za fedha zinafuatwa.
- o Kutoa kipaumbele katika kujenga uchumi endelevu wa kisasa na unaokua.

- o Kuongeza ushiriki wa wataanzania walio wengi kwenye uchumi wa taifa lao.
- o Kuandaa mazingira mazuri ya kufikisha taarifa muhimu kuhusu masoko, ubora wa viwango vinavyotakiwa na masharti mengineyo kwa wafanyabiashara na hasa wafanyabiashara wadogo na wa kati.
- o Halmashauri kutambua na kutangaza maeneo yenye vivutio vya kitalii

Maelekezo hayo hatatekelezeki na hayapimiki bila taarifa zenye takwimu sahihi.

Leo hii nimeziindua rasmi tovuti (website) ya Mkoa wa Kilimanjaro ili taarifa mbalimbali za mkoa ziweze kupatikana kote duniani kwa kufuata anwani ya tovuti hiyo (www.kilimanjaro.go.tz). Nimefurahi kupata taarifa kuwa mikoa ya Tanga, Mbeya, Manyara, Kagera, Ruvuma, Singida , Mwanza na Dar-es-salaam tovuti zao ziko hewani. Pia Halmashauri ya Ngara, Kinondoni, Ilala, Temeke na Jiji la Dar es Salaam zimeweka tovuti zao hewani.

Kupitia tovuti hizi tunaweza kupata taarifa mbalimbali za Fedha na Bajeti ; Mipango ; Kilimo na Mifugo; Maliasili na Mazingira ; Elimu; Afya; Maji; Ushirika; Biashara na nyinginezo nyingi. Safari ni ndefu na changamoto ni nyingi.

Hata hivyo pamoja na changamoto hizo natoa maagizo kwa mikoa kama ifuatavyo

1. Mikoa ambayo haijamalizia kuandaa tovuti hizi ifanye hivyo mara moja na kuweka taarifa muhimu hasa zili za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM

2. Mikoa iandae utaratibu wa kuweka taarifa humo mara kwa mara na tusiache taarifa zikae kwa muda mrefu sana bila ya kuziboresha na kuwezesha upatikanaji wake.
3. Mikoa iendeele na jitihada ya kuziwezesha wilaya ziweke taarifa zake kwenye tovuti za Mikoa.
4. Tuendeele kuhimiza matumizi sahihi ya TEKNOHAMA kuimarisha upangaji wa mipango na bajeti ; ufuatiliaji na tathmini pamoja utoaji taarifa.